

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-22-2114512, 2116898
E-mail: press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz
Faksi: 255-22-2113425



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA BARACK OBAMA,
11400 DAR ES SALAAM,
Tanzania.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ikulu, Dar es Saalam

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli amefanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC), Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma na Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma.

Taarifa iliyotolewa leo tarehe 23 Machi, 2018 na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi John Kijazi imeeleza kuwa Mhe. Rais Magufuli amemteua Prof. Lazaro S.P. Busagala kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) kuanzia tarehe 22 Machi, 2018.

Kabla ya uteuzi huo Prof. Busagala alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) - Taaluma na Utafiti.

Mhe. Rais Magufuli amemteua Prof. Damian Gabagambi kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kuanzia tarehe 22 Machi, 2018.

Prof. Gabagambi anachukua nafasi ya Bw. Mlingi Elisha Mkucha ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Kabla ya uteuzi huo Prof. Gabagambi alikuwa Mhadhiri wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Kilimo - Sokoine (SUA).

Mhe. Rais Magufuli amemteua Dkt. Deodatus Michael Mutasiwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma.

Mhe. Rais Magufuli amemteua Dkt. Alphone Bilola Chandika kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma.

Kabla ya Uteuzi huu Dkt. Chandika alikuwa akikaimu nafasi hiyo.

A blue ink signature of Gerson Msigwa.

Gerson Msigwa
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, IKULU
Dar es Salaam
23 Machi, 2018